

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
**Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo,**  
**(TaSUBa)**

Simu: 0255 023 2440032  
Nukushi: 0255 023 2440021  
Barua pepe: [tasuba@habari.go.tz](mailto:tasuba@habari.go.tz)  
Tovuti: [www.tasuba.ac.tz](http://www.tasuba.ac.tz)



S.L.P. 32,  
**BAGAMOYO**

05/11/2018

## **Taarifa kwa Umma**

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) inapenda kuutaarifu Umma ya kwamba, kuanzia tarehe 5 Novemba 2018, itahamia rasmi katika mfumo wa malipo wa Serikali ujulikanao kama Government e-Payment Gateway (GePG) kama matakwa ya sheria kwa Taasisi za Serikali.

TaSUBa ikiwa miongoni mwa Taasisi za Serikali, itanza kutumia mfumo huu kwenye makusanyo yake yote yakiwemo Ada, Ukumbi, Kodi ya pango/mabweni, Maombi ya Kujiunga na masomo, Maombi ya tenda, Maonesho na Ushauri, Tamasha n.k , **hivyo mteja atapaswa kufika au kuwasiliana na Taasisi ilikupata namba ya utambulisho wa malipo husika (Payment Control Number) kabla ya kufanya malipo.**

### **Namna ya Kulipa kwa Kutumia mfumo wa Kielektroniki (Government e-Payment Gateway):**

1. Tumia nambari ya kumbukumbu ya malipo (Control Number) uliyoipata kutoka TaSUBa kufanya malipo. Nakili namba hii ya udhibiti na tembelea Tawi lolote la Benki ya CRDB au NMB ilikulipa. Baada ya kuwasili kwenye benki, mpe mtoa huduma wa dirishani namba ya kumbukumbu ilikukamilisha mchakato wa malipo yako. Unaweza kulipa pia kwa kupitia huduma ya NMB Mobile au SIM BANKING.
2. Malipo yanaweza pia kufanywa kwa njia ya mtandao wa simu za mkononi (M- Pesa, Tigo-Pesa, na Airtel Money) kwa kufuata hatua zifuatazo:
  - a. Kutoka kwenye simu yako, piga simu \*150\*00#, au \*150\*01#, au \*150\*60# (Ili kupata Menu ya M-pesa, Tigo-Pesa, na Airtel Money kwa mtiririko huo);
  - b. Chagua "Lipia Malipo (PayBills)";
  - c. Chagua "Malipo ya Serikali";
  - d. Chagua "Ingiza namba ya malipo" na uingize namba ya kumbukumbu ya malipo (Control Number).
  - e. Weka kiasi cha fedha unachotaka kulipa;
  - f. Thibitisha muamala wako kwa kuingiza neno au namba yako ya siri;
  - g. Hifadhi ujumbe wa simu uliopokea kama ushahidi wa malipo endapo utahitajika kuonyesha kwa Taasisi.

### **Kwa maelezo zaidi, Wasiliana nasi kwa kutumia mawasiliano yafuatayo:**

- o [frank.mwombeki@tasuba.ac.tz](mailto:frank.mwombeki@tasuba.ac.tz); 0712 596 757
- o [sikalemonica@gmail.com](mailto:sikalemonica@gmail.com); 0716 072 288
- o [kilibamugisha@gmail.com](mailto:kilibamugisha@gmail.com); 0715 489 653
- o [marketing@tasuba.ac.tz](mailto:marketing@tasuba.ac.tz); 0655 840 405; 0763 275 517
- o [nzigerehema@gmail.com](mailto:nzigerehema@gmail.com); 0762 544 613; 0715 750 141
- o [peter.mayombo@tasuba.ac.tz](mailto:peter.mayombo@tasuba.ac.tz); 0718 535 585; 0784 506455

Imetolewa na:  
**MTENDAJI MKUU**